Food and Agriculture Organization of the United Nations

# JINSIA na HAKI Kuhusu Ardhi







## Kukanusha hati

Mfumo uliotumika katika kuwasilisha maelezo na ujumbe huu kamwe humaanishi kwamba maoni yoyote yaliyotolewa kuhusu Shirika la Chakula na Kilimo duniani (FAO) ama ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi (NLC) kuhusu sheria ama ustawi wa nchi yoyote, himaya, mji ama eneo ama mamlaka yake, ama kuhusu mipaka yake yana baraka za FAO na NLC. Kutaja kampuni maalum na bidhaa za baadhi ya viwanda haimanishi kwamba zimeidhinishwa na kupendekezwa na FAO ama NLC kupendelea baadhi ya majina yaliyotajwa. Maelezo katika kitabu hiki na ya waandishi wala si lazima kuwakilisha sera za FAO na NLC.

FAO inahimiza matumizi, uchapishaji na usambazaji wa habari ya kazi hii. Isipokuwa mahali ilipotoa masharti kazi hii inaweza kuchapishwa, kunakiliwa na kuchuliwa kwenye mtandao kwa mafunzo binafsi, dhamira ya utafiti na kutoa mafunzo, ama kuitumia kwa shughuli ama huduma zisizokuwa za kibiashara mradi tu kutambua FAO kama chanzo na mwenye hatimiliki na kukumbuka kuwa FAO haijadhainisha na kupendekeza mshiriki yeyote. Maombi yote ya kutafsiri ama haki za urithi na zile za kuuza tena na haki nyingine za kibiashara yanatakiwa kutumwa kupitia kwa www.fao.org/contact-us/licence, ama iwasilishwe kwa copyright@fao.org

Maelezo kuhusu bidhaa za FAO yanapatikana katika tovuti ya FAO (www.fao/publications) na yanaweza kununuliwa kupitia kwa publications-sales@fao.org

ISBN 978-92-5-009527-1 (FAO)
© FAO, 2017

**Picha zote ni kwa hisani ya afisi ya mawasiliano ya NLC.**

JINSIA na HAKI

# Kuhusu Ardhi












**Dr. Fibian Lukalo**
**Esterina Dokhe**


**2017**

# Yaliyomo


1. Kuwatambua wahusika ................................................ 6
2. Dibaji.................................................................... 8
3. Msamiti na maana ................................................... 9
4. **SEHEMU YA 1: UTANGULIZI ...................................... 18**
5 1.1 Namna ya kutumia kitabu hiki .................................... 18
6 1.2 Muktadha ............................................................. 19
7 1.3 Kuchambua mfumo wa umiliki wa ardhi na haki kuhusu mali ........................................................... 24
8. **SEHEMU YA 2 : SABABU ZA WANAWAKE NA HAKI KUHUSU ARDHI ........................................................... 28**
9. 2.0 Wanawake kumiliki ardhi ......................................... 28
10. 2.1 Wanawake kurithi ardhi ......................................... 32
11. **PART 3: MAFUNZO KUTOKA KWA SERA NA DESTURI ........ 37**
12. 3.0 Muhtasari ............................................................ 37
13. 3.1 Mikakati bora ya marebisho ..................................... 37
14. **MAREJELEO ............................................................ 40**



*“Dunia ambayo ni nzuri kwa wanawake*

# *ni nzuri kwa kila mtu’*

WELLESLEY CENTERS FOR WOMEN PHILOSOPHY

# Kuwatambua waliohusika

KUCHAPISHWA kwa kazi hii hakungekamilika bila kujitolea pakubwa kwa ufahamu na msaada kutoka kwa kurugenzi ya utafiti katika Tume ya Kitaifa ya Ardhi inayoongozwa na Clementine Kisangau, Jacinta Katee, Nancy Awere na Sheila Pamba. Kadhalika tunachukua nafasi hii kumshukuru afisa mkuu mtendaji wa Tume ya Kitaifa ya Ardhi Tom Chavangi kwa kujitolea kwake kuhakikisha kuwa kazi hii inachapishwa. Tunamshukuru mwenyekiti wa kamati ya Utafiti, Rasilimali Asili, Uhusiano Mwema na Utetezi kwa kutuunga mkono kila wakati. Wakuu wa kurugenzi tofauti, wakiwemo Bw. Elijah Letangule- Naibu mkurugenzi wa mradi wa FAO na timu yake, Bw. Francisco Carranza na Philip Kisoyan ambao wanastahili kutambuliwa kwa habari muhimu walizotoa na maelekezo ambayo yalisaidia kukamilisha kazi hii.

Shukrani za dhati zinamwendea Naibu Afisa wa Mawasiliano katika mradi huo, Bi. Nancy Cheruiyot. Tunawapongeza Prof. Juliet Macharia (Chuo kikuu cha Kirinyaga), Prof. Maurice Amutabi na Dkt. Linet Hamisi (Chuo Kikuu cha Kisii) kwa uhakiki mwaafaka waliotoa kuboraresha kijitabu hiki. Tunawashukuru makatibu wa Bodi za Ardhi katika Kaunti hasa katibu wa Kaunti ya Kakamega Carol Khasoa, timu ya Landesa kupitia kwa Diana Fletschner na Jennifer Duncan kwa maoni na dhana zao ambazo tumezijumuisha. Kadhalika kundi la Equity Resource likiongozwa na Renee Giovarelli lilitoa maarifa muhimu na msukumo wa 'Kutoa sauti ya wanawake kuhusu masuala ya ardhi'. Kadhalika tunawashuru wahakiki wawili ambao hawakutaka kutajwa kwa kutoa maoni bora yaliyotumika katika kuboresha kazi hii.

Shukran za dhati tunazitoa kwa Muungano wa Ulaya kwa ufadhili wa pesa na Shirika la Chakula na kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kwa maelekezo na kutuhimiza wakati wa kuandaa kijitabu hiki. Kuna wengine wengi kina mama, kina baba, wake na waume, ndugu na dada na mashangazi ambao walitupa hamasa katika mchakato wetu wa kuchapisha kitabu hiki. Vituo vya Wellesley kuhusu Falsafa za Wanawake 'Dunia ambayo ni bora kwa wanawake ni nzuri kwa kila mtu ' inasisitiza msukumo wa kuchapisha kazi hii. Bw. Franklin Ongeti, tunakuipongeza kwa usanifu wa kurasa za chapisho hili. Mwisho, tunamshukuru Bw. Wattuman Memba kwa marekebisho aliyoyafanyia kijitabu hiki.

# Dibaji

Kwa zaidi ya miaka miwili baada ya kuzinduliwa kwa Tume ya Kitaifa ya Ardhi Februari 2013, hatua nyingi zimepigwa za kuboresha usimamizi wa ardhi nchini Kenya. Kuchapisha kitabu hiki ni ufanisi unaohitaji kusherehekea kwa sheria na kanuni mbalimbali zilizobuniwa katika kuzindua katiba ya Kenya inayolenga marekebisho katika sekta ya ardhi ambayo yamewekwa kukidhi mahitaji ya usawa wa jinsia katika masuala ya ardhi.  Katiba mpya ndiyo kilele cha ongezeko la hatua zilizopigwa na nchi ili kuinua hadhi ya wanawake na maslahi yao katika ardhi. Katiba mpya inawakilisha hatua kubwa zilizopigwa kuboresha hadhi za wanaume na wanawake katika nyanja zote za maisha. Kwa sababu hiyo pana haja ya kuzingatia ufafanuzi wa ardhi kwa upana (maji na nafasi iliyopo) kama rasilimali asilia na mali nyingine inayopatikana katika ardhi. Ardhi na mali nyingine (kama mifugo, madini yanayochimbuliwa, mashine na kadhalika.) inaweza kutumika kwa kilimo na uzalishaji na vile vile inaweza kuwa chanzo cha uwezeshwaji wa kisiasa miongoni mwa wanawake. Kuwa na uwezo wa kupata ardhi na mali kunatoa nafasi ya makazi na kuwawezesha wanawake kujiunga katika ushindani wa siasa kuhusu rasiliamali; ardhi ni mali inayostahili kujumuishwa katika ndoa na inaweza kutumika kama chombo cha kupata mikopo. Muhimu kutaja kuwa ardhi na mali ndiyo msingi wa kuwawezesha wanawake wengi kiuchumi na kuwapa ukakamavu wa kufanya maamuzi na kupigania haki zao kwa rasilimali lakini pia kuwapa 'utulivu wa moyo"

Kitabu hiki kimeorodhesha fursa na mapendekezo ili ikiwa wanawake watahitajika kutoa mchango wao kikamilifu katika jamii ya Wakenya, wanatakiwa kuchangamikia utaratibu uliowekwa wa kisheria katika utekelezaji wa katiba mpya kwa uzito.

**Tom Aziz Chavangi**
**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Tume ya Kitaifa ya Ardhi**

# Msamiati na Maana

| MSAMIATI | MAANA |
|---|---|
| **Hati kamili** | Hati chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 300 (iliyoondolewa) ya ardhi inayomilikiwa kikamilifu. Hii ni namna ya umiliki ambayo mwenye ardhi anakuwa na haki zote kuhusu muda wa kuimiliki na matumizi ya ardhi hiyo. |
| **Kupata ardhi** | Haki ya kuingia katika na kuitumia ardhi. Haki hizi si za kudumu na zinaweza kupeanwa kwa mwanume ama mwanamke katika familia ama ukoo. |
| **Barua ya kukabidhi ardhi** | Cheti kinachothibitisha kuwa dhamana zote za aliyetuma maombi zimezigatiwa na pia inaonyesha haki zake katika kipande hicho cha ardhi |
| **Posa** | Pesa, mali, ama huduma ambazo zinalipwa na anayeposa ama familia yake kwa familia ya anayeolewa. |
| **Cheti cha kukodisha** | Hii ni stakabadhi inayoonyesha mfumo wa umiliki wa ardhi kwa njia ya kukodisha ambapo anayekodishiwa ana haki ya kuwa na ardhi hiyo kwa muda maalum na atazingatia masharti yaliyowekwa na anayakodisha (mwenye ardhi). |
| **Cheti cha hati** | Chini ya sura ya 281 hutolewa ili kugawanya ardhi bila kubadilisha jina la mtumizi. Mabadiliko ya mtumizi hutokea baada ya kugeuza namna ardhi hiyo ilivyokuwa ikitumika, kwa mfano kutoka kwa kilimo hadi kwa sehemu ya makazi. |
| **Mabadiliko ya Anga** | Haya ni mabadiliko ya hali ya hewa katika eneo fulani ama duniani. Mabadiliko hayo hubadilisha mfumo wa anga kwa jumla unaojumuisha kama kiwango cha mvua, halijoto, mawingu na kadhalika. |
| **Umiliki wa kawaida** | Namna ya kumiliki ardhi kwa pamoja. Zaidi ya mtu mmoja ama kundi la watu kumiliki ardhi ama mali nyingine – kila mtu anamiliki sehemu ya ardhi hiyo kubwa, hugawanywa kwa |

| | |
|---|---|
| | usawa isipokuwa kama kuna sababu nyingine |
| **Umiliki wa kundi** | Huu ni umiliki wa pamoja. Kundi linakuwa na haki za kipekee za kumiliki na kusimamia na /ama kutumia ardhi na rasilimali asili. |
| **Jamii** | Kundin la kijamii ama kidini ambalo linaishi katika eneo fulani, mara nyingi yana tamaduni na historia asilia zinazofanana, wana sifa zinazofanana, maslahi yao yanalingana kwa sehemu kubwa ya jamii inayoangaziwa. Inaweza pia kuashiria sehemu ambayo inaishi jamii hiyo. |
| **Ardhi ya jamii** | Ni ardhi inayomilikiwa na jamii na hutambuliwa kwa misingi ya kabila, tamaduni ama jamii yenye maslahi sawa. |
| **Maslahi yanayoshindana** | Wakati makundi tofauti yanapingania maslahi sawa katika kipande cha ardhi (kwa mfano ikiwa pande mbili zinadai kikamilifu haki za kutumia ardhi ya kilimo. Mzozo wa ardhi hutokea katika ushindani huo.) |
| **Maslahi yanayofanana** | Wakati makundi tofauti yanapokuwa na maslahi sawa katika kipande kimoja cha ardhi (kwa mfano watu wa jamii moja wakiwa na haki sawa katika ardhi ya kulisha mifugo na kadhalika.) |
| **Kutwaa kwa lazima** | Nguvu za serikali kutwaa haki za watu binafsi kumiliki ardhi bila idhini kutoka kwa mmiliki ama mtumizi wa ardhi kwa manufaa ya jamii. |
| **Makubaliano ya kuishi** | Watu wawili wanaamua kuishi pamoja kama wanandoa lakini uhusiano wao hautambuliwi kisheria |
| **Haki za kuthibiti** | Haki za kutoa maamuzi kuhusu namna ardhi inatavyotakiwa kutumika na kuamua mimea inayostahili kukuza na kufaidika kutokana na mauzo ya mavuno na kadhalika. |
| **Sheria ya kitamaduni** | Hizi ni sheria ambazo zinazingatia utamaduni na zinaweza kuathiriwa na maoni ya umma katika jamii fulani kuhusu tabia ama itikadi |

**Kuwa na uthibiti kuhusu ardhi** Uwezo wa kutoa maamuzi kuhusu ardhi (Kwa mfano kuamua kiwango cha ardhi kitakachotumiwa kwa shughuli za kilimo na ikiwa ardhi hiyo itatumika kuzalisha vyakula ama mime ya kuuza) ana uwezo wa kuhamisha hati miliki za ardhi kwa kuuza ama kurithi i (umiliki wa ardhi).

**Ubaguzi** Ni namna ya kumtenga mtu kushiriki katika kikundi ama kitengo fulani. Inahusisha tabia halisi kwa makundi kama vile kuwatenga ama kuwawekea vikwazo watu wa kundi fulani kunufaika kwa jambo ambalo kundi jingine linafaidika.

**Mahari** Pesa, bidhaa, ardhi ama mali nyingine ambayo mwanamke analeta katika ndoa: mara nyingi inalipwa na familia atakayoolewa na wakati fulani inalipwa kwa familia ya mwanaume anayeoa.

**Haki ya mwingilio** Kuwa na haki ama maslahi katika ardhi ambayo inamilikiwa na mtu mwingine na huwa na mzigo mkubwa katika ardhi hiyo. Kutumia ardhi hiyo katika namna fulani na itamhitaji mwenye ardhi kutumia sheria inayohusiana na ardhi ama kuwekea masharti ya matumizi kwa mutumiaji na haitajumuisha faida.

**Usawa na usawazishaji** Usawa unalenga kuanzishia kwa kituo kimoja kwa kila mtu. Usawazishaji ni kuwa na lengo la kuhakikisha kila mmoja anafaidika kikamilifu kufikia mwisho wa jambo fulani.

**Kutwaa:** Haki ya kutwaa ardhi ama nyumba ya mkopo ikiwa mpangaji ama anayenunua amekiuka yaliyomo kwenye mkataba

**Umiliki kamilifu** Kumiliki ardhi ama mali bila kuwekewa vikwazo ama vipimo vya muda. Mfumo huonyesha kuwa anayemiliki ana usemi wote kuhusu ardhi na inampa mamlaka kamili ya umiliki wa ardhi hiyo.

**Jinsia** Uhusiano kati ya wanaume na wanawake jinsi wanavyochukuliwa kadhalika kama mali. Jinsia haimuliwi

kibayolojia kutokana na sifa za kike ama kiume bali kijamii. Ni nguzo muhimu ya jamii mbalimbali na huongoza mipangilio ya kuzalisha, kuzaa na kuzalishwa, utumizi na usambazaji (maelezo kutoka FAO).

**Usawa wa jinsia** Utaratibu wa kugawanya rasilimali, miradi na kutoa maamuzi ya haki kwa wanawake na wanaume bila ubaguzi kwa kuzingatia jinsia na kushughulikia tofauti zilipo kwa manufaa ya wanaume na wanawake.

**Ubaguzi wa kijinsia** Namna dhalilishi na matokeo yanayowanyima wanawake haki ya kufurahia haki zao za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na maendeleo. Ni kinyume cha maadili ya utu, uhuru na ulinzi miongoni mwa wanaume na wanawake.

**Uhusiano wa kijinsia** Ufafanuzi wa kijamii' kuhusu wanawake na wanaume. Hii inatofautiana kutoka kwa jamii na tamaduni, hadhi katika jamii, umri na nyakati tofauti katika historia. Kuna majukumu maalum ya kijinsia ambayo huathiriwa na muundo wa familia, kufikia rasilimali, athari maalum kwa uchumi wa dunia, na masuala mengine ya kimsingi kuhusu mazingira.

**Majukumu ya kijinsia** Hii ni namna utamaduni ama jamii inavyofafanua haki, majukumu na utambulisho wa wanaume na wanawake na uhusiano kati yao

**Kadi ya kijani(Green Card)** Ni stakabadhi inayoweka rekodi halisi za mikataba iliyofanywa katika kipande cha radhi/ploti..

**Mfumo wa upangaji** "Inahusiana na upangaji", inaamaanisha mali chini ya upangaji.

**Nyenzo** Ni stakabadhi inayowezesha utekelezaji wa haki za usawazishaji na anayestahili kuwajibishwa.

**Maslahi** Kuwa na haki katika ama juu ya ardhi na mali.

**Umiliki wa pamoja** Namna ya kumiliki mali zaidi ya mtu mmoja ama umiliki wa kisheria wa ardhi ama mali nyingine– kila mtu anamiliki

jumla ya mali hiyo ambayo haigawanywi.

**Ardhi** Kwa mujibu wa katiba ya Kenya: inatambua mahali halisi ilipo mali hiyo ama sehemu ya mali hiyo juu ya mchanga wa dunia, bidhaa iliyo chini, hewa iliyo juu yake na vitu ambavyo viko katika mchanga huo.

**Uongozi katika masuala ardhi** Utaratibu wa kuamua, kunakili, kubadilisha na kusambaza habari kuhusu umiliki, thamana na matumizi ya ardhi

**Usimamizi wa ardhi** Ni utaratibu wa kusimamia matumizi na ustawishaji wa rasilimali za ardhi

**Marekebisho katika sekta ya ardhi** Inajihusisha na mabadiliko kuhusu haki ya kumiliki mifumo mbalimbali ya ardhi na kugawanya upya ardhi kwa kuzingatia malengo ya kisiasa yaliyomo katika marekebisho yaliyowekwa.

**Sajili ya ardhi:** Huu ni mfumo ambao unashughulikia masuala ya umiliki. Umiliki ama haki nyengine kuhusu ardhi zinaweza kunakiliwa ili kutoa ushahidi kuhusi umiliki kupitia kwa hati miliki

**Mfumo wa ardhi** Uhusiano wa watu kibinafsi ama makundi kwa mujibu wa ardhi. Inaonyesha namna haki kuhusu ardhi zinavyotekezwa, namna ya kuzilinda haki hizo katika kumiliki ardhi ambayo mara nyingi hutumika katika shughuli mbalimbali, na pia haki za kisheria.

**Haki za mfumo wa ardhi** Hizi ni haki za kisheria zinazoonyesha uhusiano baina ya watu, wanaweza kuwa watu binafsi ama makundi na ardhi. Hii ni zaidi ya haki rasmi zinazojumuisha haki za kitamaduni.

**Hati ya shamba** Ushahidi wa maandishi kuonyesha haki ya mtu ya kumiliki ardhi ama umiliki wenyewe kwa kutegemea muktadha.

**Matumizi ya ardhi** Matumizi ya ardhi yanaambatanishwa na mikataba, shughuli na uwekezaji wanaofanya watu katika ardhi fulani katika hali ya kuzalisha, kubadilisha ama kuiacha ilivyo.

**Thamana ya ardhi** Thamani ya ardhi huamuliwa kwa njia nyingi ili kutoa

makadirio kamili ya thamani hiyo.

**Kukodisha** Anayemiliki mali ya mtu mwingine kwa malipo ama bila malipo ya fedha kwa kipindi fulani. Mfumo huo wa kukodesha unaweza kuwa wa kusajiliwa, usiosajiliwa, muda mrefu ama mfupi.

**Umiliki wa kukodisha** Ni maslahi yanayowekwa katika ardhi kwa kipindi cha miaka fulani.

**Mkodishwaji** Mtu anayekodisha ardhi, jengo ama ploti.

**Mkodishaji** Mtu anayemiliki ardhi.

**Barua ya kibali** Barua inayoonyesha kanuni na masharti ya kununua nyumba ama ploti. Barua hiyo mara nyingi huandikwa kabla ya malipo yoyote kufanywa na kuwekwa saini na mnunuzi na muuzaji.

**Ndoa** Ya serikali, kitamaduni ama ya dini

**Mali katika Ndoa:** Hii inajumuisha boma ama maboma ya wanandoa, bidhaa za nyumbani na athari katika boma hilo ama mali yoyote inayoweza kusongezwa ama kutohamishwa ambayo ilipatikana na kumilikiwa kwa pamoja wakati mume na mke wakiwa pamoja katika ndoa.

**Ugavi wa ardhi** Kugawanya ardhi katika vipande vidogo vidogo.

**Maslahi yanayolandana** Hapa makundi kadhaa yanapewa haki tofauti katika kipande cha ardhi (kwa mfano sehemu moja inaweza kupewa haki ya kukodisha na nyingine ipewe haki ya kutoa uamuzi wa mwisho na kadhalika.)

**Maslahi yanapingana:** Ni maslahi ya kisheria ya ardhi ambayo yana msukumo wa kisheria japokuwa hayajanakiliwa katika sajili ya umma ya ardhi; taifa ama jamii ina uwezo wa kugawa ama kugawanya upya ardhi ya kibinafsi iliyochukuliwa, na kadhalika.

**Haki endelevu:** Sawa na haki za kumiliki ardhi kikamilifu; ni haki za kumiliki ardhi bila muda wa masharti ama kuimiliki milele.

**Maelekezo:** Umiliki unaozaniwa ama haki za kumiliki ardhi bila idhini, kwa ujeuri na kuendelea kumiliki ardhi hiyo kwa miaka kumi na

miwili.

**Mali:** Inajumuisha ardhi na kile kilichowekezwa juu yake.

**Mmiliki:** Kwa mujibu wa ardhi ama kukodisha, mtu aliyetajwa katika afisi ya usajili wa ardhi kama mmiliki ama anayestahili kusimamia wakati uamuzi huo ulipofanywa.

**Ardhi ya umma** Hizi ni ardhi ambazo ziko chini ya serikali kuu na zile za kaunti kwa mujibu wa sheria.

**Ardhi ya kibinafsi:** Hii inajumuisha ardhi inayomilikiwa na mtu yeyote chini ya umiliki kamilifu wa ardhi: na ardhi mbayo inamilikiwa katika mfumo wa kupanga;

**Hati ya Masharti:** Inaonyesha serikali ina haki kamilifu ya kumiliki ardhi fulani. Hapa ni wakati serikali ina haki zote za kutwaa ardhi yoyote inayoitaka katika mipaka yake kwa lazima. Hati hii ya lazima kutoka kwa serikali inatokana na dhana kuwa serikali ina uwezo wa kujitawala kwa njia huru katika mipaka yake. Huu huwa uamuzi wa mwisho unaotolewa na serikali ambapo haki mbalimbali za umiliki zinapuuzwa. Ni hati kamilifu ya serikali ambayo haionekani kuwa na manufaa lakini imejikita kwa uongozi na umiliki unaotegemea serikali kuwa uhuru na kujitwala

**Haki za ziada kuhusu ardhi :** Wanawake wana hizi haki kuhusu ardhi ila ni kupitia kwa jamaa wa kiume kutoka familia zao. Hivyo basi wanawake wamo katika hatari ya kupoteza Mali Yao kukitokea talaka, ujane ama waume wao kuhamia kwengine.

**Hati ya sehemu**: Hii ni hati ya sehemu ya jengo kwa mfano katika jumba la orofa kadhaa. Inatokana na Sheria ya kumiliki sehemu ya mali ya 1987 na hati hiyo kusajiliwa chini ya Sheria ya kusajili ardhi, Sura ya 300. Ni muhimu kukumbuka kuwa Sheria ya kusajili ardhi ya 2012 katika Sehemu ya 26 inajumuisha aina mbalimbali ya hati zilizoangaziwa hapo juu na kuwa Cheti cha Hati. Madhumuni yalikuwa kupunguza utata ulioletwa na Sheria za awali za ardhi ambazo

zilisababisha kuwepo kwa mkanganyiko kwa aina za hati zilizokuwepo.

**Usimamizi enedelevu wa ardhi**: Kutumia rasilimali za ardhi zinazojumuisha mchanga, maji, wanyama na mimea kwa kuzalisha bidhaa ili ufikia mahitaji ya binadamu yanayobadilika mbali na kuhakikisha wakati huo huo kuwa kuna uwezekano wa uzalishaji wa muda mrefu wa rasilimali hizi na kulinda mazingira.

**Upangaji:** Inamaanisha uhusiano uliowekwa na ukodishaji.

**Mkataba wa upangaji:** Namna ya mkataba wa maandishi ama mazungumzo kati ya mpangaji na mwenye nyumba kuhusu kuingia kwa makazi ama jingo la kibishara ambayo inajumuisha leseni ya kulitumia jengo hilo kwa ada. Huthibiti uhusiano kati ya mwenye nyumba na mpangaji.

**Hati miliki** Ni mkataba uliotiwa saini ambao unathibitisha umiliki wa ardhi na haki za kisheria zinazojumuishwa..

**Haki za uhamisho** Haki ya kuuza ama kutoa ardhi kwa kulipia polepole, kuhamisha ardhi kwa watu wengine kupitia kwa kugawanya baina ya wanajamii na kuhamisha ardhi hiyo hadi kwa warithi na kuamua namna itakavyotumika na haki za kuthibiti.

**Mali ya amana** Mali inayomilikiwa na mume ama mke kama amana ikiwa ilipatikana kwa urithi ama vinginevyo

**Haki za matumizi** Haki ya kutumia ardhi kwa malisho ya mifugo, kukuza mimea, na kukusanya bidhaa za msitu na kadhalika.

**Haki za maji** Inashughulikia kutoa (na kisha kutumia) maji kutoka kwa mazingira asili ama kuyatumia katika mazingira hayo. Haki ya maji ni haki ya kisheria na inajumuisha kutiririka kwa maji.

**Haki za kuthibiti** Haki za kutoa maamuzi kuhusu namna ardhi inatavyotakiwa kutumika na kuamua mimea inayostahili kukuza na kufaidika kutokana na mauzo ya mavuno na kadhalika.



*"Ikiwa unauza ardhi ya baba yako Ili ununue tarumbeta utasimama wapi kuipuliza? (Methali ya Cameroun)*

# Sehemu ya Kwanza: Utangulizi

## 1:1 JINSI YA KUTUMIA KITABU HIKI

KITABU HIKI kimeandaliwa kumsaidia yeyote ambaye ana haja ya kuelewa masuala tata na mazito kuhusu ardhi nchini Kenya. Kumekuwa na ukiukaji mkubwa wa haki katika suala zima la ardhi hasa katika haki za wanawake kuhusu ardhi. Kuwa na mtazamo kuhusu masuala wanawake kumiliki ardhi ni muhimu kama alivyosema Kate Lines (2015): Mabadiliko hayatatoka kwa kutambua suala hilo ila kwa kubadilisha mielekeo yetu, tamaduni na ufahamu. Hii itatokana na uongozi bora na mashauriano ya kina yanayatakiwa kufanywa.

Kadhalika inatabiriwa kuwa maafisa wa serikali ya kitaifa na zile za Kaunti (serikali za kaunti na Bodi za usimamizi wa ardhi za kaunti); makundi ya mashinani; watunga sera; watetezi wa haki za ardhi na wataalamu wa maendeleo wanaotaka kuandaa mipango ya kuwasaidia wanawake ambao wanategemea ardhi moja kwa moja watapata habari katika kitabu hiki ufumbuzi wa muhimu sana katika kazi zao

## 1:2 KULINGANA NA MUKTADHA

KENYA INA kilomita 582,646 mraba ya ardhi ambayo katiba ya Kenya ya 2010 imeorodhesha kama ya **umma, ya kibinafsi ama ardhi ya jamii.** [1] Ardhi ya umma ni kilomita 77,792 mraba (13%); Ardhi ya kibinafsi ni kilomita 107,953 mraba (19%) na kilomita 396,315 mraba ya jamii (68%), (GoK, 2013: 1). Jedwali 1 linaonyesha aian

tatu za mifumo ya ardhi ambayo inazingatia haki hizo.

**Jedwali 1:0 Mifumo ya Ardhi**

| Aina | Maelezo | Vipengee vya katiba | Sheria za Ardhi |
|---|---|---|---|
| **Ardhi ya umma** | Inajumuisha, ardhi iliyotengwa kwa matumizi ama kumilikiwa na asasi ya serikali, mbuga za kitaifa na mbuga ndogo za wanyama. Pia inajumuisha barabara kuu, mito/maziwa na bahari na ardhi nyingine ambayo haijaorodheshwa kama ya kibinafsi ama ya kijamii chini ya katiba. Ni aina fulani ya ardhi ya umma huamua ikiwa watu katika nchi wataikabidhi kwa serikali ya kaunti ama wakenya kuitoa kwa serikali kuu. | -Kipengee 62 | Katiba ya 2010<br><br>-Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi, 2012<br><br>-Sheria ya Ardhi, 2012 |

1 Draft Community Land Bill under deliberation by the Parliament – 2015.

| Aina | Maelezo | Vipengee vya katiba | Sheria za Ardhi |
|---|---|---|---|
| **Ardhi ya jamii** | Hii ni ardhi ya kijamii ambayo hutambuliwa kwa misingi ya kabila, utamaduni ama jamii yenye maslahi sawa. Ardhi ya kijamii inajumuisha:<br><br>i. Ardhi iliyosajiliwa kisheria kwa jina la wawakilishi wa kikundi ama ihamishwe hadi kwa kundi Fulani la kijamii<br>ii. Ardhi za vizazi na zile zilizokaliwa kidesturi na jamii za wawindaji na zilizokuwa zikiishi msituni.<br>iii. Kusimamia ardhi na jamii fulani kama msitu, maeneo la malisho na sehemu na mivigha (sehemu teule zinazofanyiwa maombi ama matambiko).<br>iv. Ardhi aambayo serikali za kaunti zimepewa amana juu yake–haijumuishi ardhi yoyote ya umma ambayo imewekewa amana<br>v. Ardhi iliyoamuliwa kuwa ya jamii na bunge. | -Kipengee cha 62 | -Katiba 2010<br>-Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi, 2012<br>-Sheria ya Ardhi, 2012 |

| Aina | Maelezo | Vipengee vya katiba | Sheria za Ardhi |
|---|---|---|---|
| **Ardhi ya kibinafsi** | Ardhi ya kibinfsi inajumuisha ardhi iliyosajiliwa na mtu chini ya umiliki kamilifu ama ya kukodisha na ardhi yoyote ile iliyotangazwa kuwa ya kibinafsi chini ya sheria ya bunge. | -Kipengee 64 | -Katiba ya 2010<br>Sheria ya Tume ya kitaifa ya Ardhi, 2012<br>-Sheria ya |

Kiwango cha ardhi ya umma na ile ya jamii kinatarajiwa kupunguka kwa sababu ardhi imeanza kuhusishwa na watu binafsi ama taasisi katika masuala ya kukodisha. Hivyo basi, ardhi zaidi itasajiliwa kupitia kwa maamuzi kuhusu ardhi. Kiwango cha ardhi ya kibinafsi kinatarajiwa kuongezeka kwa sababu ardhi kubwa ya kijamii itasajiliwa na ardhi kubwa ya umma itakuwa imechukuliwa. (Serikali ya Kenya, 2013:1).

Athari za kijinsia kuhusu yaliyotajwa hapo juu zinapungua ama kuongezeka kulingana na mifumo ya ardhi ambayo ni tofauti. Hata hivyo kilicho dhahiri ni kwamba haki kuhusu ardhi bila kujali mfumo wa ardhi wenyewe zinaambatana na haki ya kupata chakula, haki ya kufanya kazi mbali na haki nyingine za kibinadamu. Hivyo basi, ardhi kama mojawapo ya vyombo vya uzalishaji ni rasilimali muhimu ambayo Kenya inamiliki. Ni muhimu katika ufanisi wa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Ardhi inatajwa kama chimbuko kuu la maisha na mali inayoonekana kwa kubeba rasilimali asilia. Kutumia ardhi na ulinzi wa ardhi wake pamoja na usimamizi wake huwa na athari kubwa za kimaendeleo

Uchumi wa Kenya unategemea kilimo kwa kiasi kikubwa, ambapo 80% ya watu wanaendelea kuishi mashambani na maisha na ajira zao hutokana na shughuli za kilimo.Ardhi huzifaa jamii za mashambani kwa vyakula vya kimsingi vinavyowawezesha kuishi na pia kuviuza sokoni. Inatoa msingi imara ambapo nyumba zinaweza kujengwa kukidhi maslahi ya watu na kupanga mikakati ya kimaisha. Mara nyingi haki za kumiliki ardhi huegemea utambulisho wa jamii, umuhimu wake na jambo linaloweza kudumu kwa siku nyingi.

Kipengee 61(1) cha katiba ya Kenya (2010) kinasema kuwa ardhi yote nchini Kenya inamilikiwa na wananchi kama vile ardhi ya kitaifa, ya kijamii na watu binafsi. Katika muktadha huo, sera saba zinazotoa muongozo wa ardhi zilizomo kata Sera ya Ardhi ya mwaka wa na vilevile zilizopo katika katiba ya mwaka wa 2010 zinalenga kuimarisha usimamizi wa maswala ya ardhi nchini Kenya .

Miongoni mwa sera hizi ni

1. Kuhakikisha usawa katika ugavi wa ardhi
2. Kuhimiza matumizi mazuri ya ardhi na yenye faida
3. Kuhakikisha uwazi katika usimamizi wa ardhi kwa gharama ya chini
4. Ulinzi wa maeneo yanayofaa kuhifadhiwa
5. Kuondoa unyanyapaa wa kijinsia katika sheria ,mila na taratibu zinazohusu ardhi
6. Kuhimiza jamii kutatua mizozo ya ardhi katika njia zinazotambuliwa katika jamii hizo na
7. Kulinda haki za wamiliki

Licha ya sera hizo kuwekwa wazi, suala la ardhi nchini Kenya limekuwa donda sugu kufuatia wingi wa wanaodai kumiliki ardhi na raslimali nyengine zinazohusiana na ardhi (Kameri-Mbote2014).

Utatuzi wa masuala ya ardhi kati ya wanawake na wanaume ni mojawapo ya matatizo yanayokabili maendeleo. Jambo hili ni la dharura hasa tukizingatia mabadiliko katika idadi ya watu, miktadha ya kijamii mbali na ushindani wa maslahi katika ardhi na rasilimali asili. Maslahi haya yanayokinzana yanatokea kwa muktadha wa mfumo wa ardhi unaotambuliwa katika Jedwali 1.1, na kuorodheshwa katika katiba ya 2010.

**Jedwali 1:1 Mifumo ya umiliki wa ardhi nchini Kenya**

| MFUMO WA UMILIKI WA ARDHI | MAELEZO |
|---|---|
| **Umiliki wa ardhi** | Je umiliki wa rdhi hii unajumuisha kupitisha haki za umiliki kupitia kurithi? Mwenye ardhi anaweza kuwa aliipata kwa kununu ama kurithi. |
| **Mfumo wa ukodeshaji** | Huu ni umiliki wa muda wa ardhi kupitia kwa ada ya kulipa kodi kwa ardhi. Hii ni sawa na kupangisha nyumba na kumlipa mmiliki wa nyumba hiyo ada mliokubaliana bila wewe kumiliki nyuba hiyo. |
| **Mfumo wa umiliki usiokuwa na maslahi kamili** | Ardhi ambapo kuna maslahi tofauti ya washikadau katika kipande fulani cha ardhi. Hii inaweza kujumuisha kurahisishwa wakati mtu mmoja ana haki katika baadhi ya sehemu za ardhi ya mtu mwengine. Mifano ya mfumo wa ardhi isiyokuwa na maslahi kamili inajumuisha taratibu za serikali za kutenga ama kukubaliana na watu binafsi na / ama makundi ya umma. |
| **Mfumo wa umiliki wa kitamaduni** | Umiliki hapa ni kupitia kwa tamaduni. Katiba haitambui mfumo wa kitamaduni ikiwa unakikuka na matakwa na kanuni zilizowekwa kwa Katiba kuhusu masuala ya kutorithi kwa sababu ya jinsia. Miaka mingi ya kukodisha ardhi ni miaka 99, ambayo ni mabadiliko makubwa kutoka kwa miaka ya awali 999 waliostahili kukodisha ardhi wananchi. Mtu asiyekuwa raiya anaweza tu kuwa na ardhi kupitia mfumo wa kukodisha ambayo ni tofauti na mfumo wa zamani ambao uliwaruhusu wageni kumiliki ardhi muhimu. Matakwa mapya ya ardhi kuhusu katiba yanafanya raiya wengi kuweza kupata ardhi na kusaidia kupunguza kiwango cha umasikini nchini. |

Kwa mujibu wa mfumo wa umiliki wa kitamaduni[3] hapo juu kutokana na kilichopatikana katika kaunti ya za Narok na Kajiado kwa kuzingatia baadhi ya ranchi:

3 Makala yaliyochapisha ya Lorenzo Cotula (Ed.)(2007) ' Changes in 'customary' land tenure systems in Africa, yanaangazia namna mbalimbali mfumo wa ardhi za kitamaduni umefanyiwa mabadiliko ambayo bado yanadhulimu makundi ya wanawake.

Huku thamana ya ardhi inapoongezeka kutokana na kuwepo kwa bidhaa nyingine zinazowezwa kuhamishwa (kwa kulinganisha mifugo kama ng'ombe na mbuzi katika jamii ya Wamaasai), mfumo ambao ulionekana kufanya kazi kwa usawa chini ya sheria za umiliki wa ardhi kitamaduni huenda sasa usiwe na usawa. Badala yake visa vya ukosefu wa ardhi na wanawake kutorithi mali waliopata kwa ndoa vinazidi kuongezeka.

## 1:3 KUCHAMBUA MFUMO WA UMILIKI WA ARDHI WENYE DHAMANA NA HAKI ZA KUMILIKI MALI

MFUMO WA UMILIKI wa ardhi unaweza kufafanuliwa kama masharti ambayo ardhi imo, inavyotumika na shughuli zinazofanyiwa hapo. Marekebisho katika mfumo wa umiliki wa ardhi ni mabadiliko yanayofanywa katika masharti na hali (kwa mfano kubadilisha kwa masharti ya kandarasi kati ya wamiliki wa ardhi na wanaokodisha ama kubadilisha mfumo wa upangaji ambao hukuwa rasmi hadi katika hali rasmi ya haki za kumiliki mali).

Lengo muhimu ni kuhakikisha na kulinda haki za watu za kumiliki ardhi. Hii inaweza kuwa muhimu kwa mujibu wa kujiepusha na kuhamishwa kwa nguvu na kukosa ardhi. Kadhalika, inaweza kuwa muhimu kwa haki za wamiliki wanaotaka kuwekeza katika ardhi na kuitumia kujiendeleza kwa muda mrefu. Mfumo wa umiliki wa ardhi unaonyesha uhusiano uliopo wa kitaasisi kati ya watu kwa mujibu wa ardhi – mfumo wa kumiliki ardhi kikamilifu, mfumo wa kukodisha ardhi, mfumo wa maslahi yasikuwa kamilifu na mfumo wa kitamaduni wa kumiliki ardhi. Uhusiano huo unaonyesha namna haki zinavyomilikiwa, kutumia, kufikia, kuthibiti, kuhamisha na kusimamia ardhi.

Kuna jinsi aina mbalimbali masuali ya kimsingi yanayostahili kuulizwa tunaporejelea matatizo wanayokumbana nayo wanawake na makundi yaliyotengwa kuhusu umiliki wa ardhi. Hii ni kama yafuatavyo:

a. **Kijamii na kiutamaduni:** Je, haki kuhusu ardhi zimewekwa katika uhusiano mpana wa kijamii na kitamaduni? Je, kuna athari gani ya muundo wa haki kuhusu ardhi kwa ubaguzi wa kijinsia katika maisha ya wanawake? Kuna vile mfumo wa umiliki wa ardhi unaohusishwa na hadhi, rangi, kabila na/njia

nyingine za ubaguzi? Je, haki kuhusu ardhi ni msingi muhimu wa dhamana kwa watu masikini? Je, mifumo ya zamani ya kumiliki ardhi imeathiriwa vipi na sheria za kikoloni ama baada ya ukoloni? Je, mageuzi ya sera yanaambatana vipi na michakato inayoendelea isiyokuwa rasmi?

**b. Kisheria:** Je, mifumo katika sheria na katiba inaathiri umiliki wa ardhi nchini? Je, kuna njia sahihi na zilizo sawa kisheria kutumika katika hali zinazohusu umiliki wa ardhi mijini na mashambani? Kuna Sheria zipi zinazohusu umiliki wa ardhi kwa jumla? Ni wakati upi na wapi ambapo mipango ya usajili na uandikishaji hati unafaa? Je, wamiliki wa jumla wanahitaji kusajiliwa na kupewa hati miliki?

**c. Kiuchumi:** Ni jinsi gani mifumo ya ugavi wa ardhi inaathiri ukulima na njia nyenginezo za mapato? Je, ardhi inayomilikiwa kwa jumla ina manufaa yapi kiuchumi? Ni vipi mfumo wa ugavi wa ardhi unavyoingiliana na mauzo ya ardhi, mahitaji, kazi na matokeo? Je, kutokuwepo kwa uwazi katika maswala ya umiliki wa ardhi kunawavunja moyo wawekezaji?

**d. Kisiasa:** Je, umiliki wa ardhi ni tofauti na usimamizi wake, kwa mfano wakati mpangaji na mmiliki hawasikizani? Ni vipi marekebisho katika mifumo ya kumiliki ardhi inahusiana na marekebisho katika mageuzi yahayohusu ardhi kwa jumla? Je, hali za kisiasa zinaruhusu mageuzi katika mifumo ya umiliki wa radhi?. Je, uendeshaji wa mipango ya ardhi nchini imefanikiwa kitaifa, kikanda na mashinani?

Umiliki wa ardhi unafaa kueleweka kama mkusanyiko wa haki za umiliki wa ardhi kama zilivyoandika katika mchoro 1:0 hapo chini.

**Mchoro 1:0 Haki za umiliki wa ardhi na mali**



**Kulingana na mchoro 1:0 hapo juu ni muhimu kuzingatia sababu muhimu zilizotolewa ifuatavyo:**

a. Mfumo wa ardhi unaweza kutajwa kuwa wenye dhamana ama usiokuwa na dhamana;

b. Mfumo wa dhamana ya ardhi unaweza kueleweka kwa maana nyingi ; badhi ya sababu zinazoweza kuathiri ulinzi huo zinajumuisha upana; ukubwa na muda uliowekwa kuhusu haki za ardhi ; ukubalifu wa haki kuhusu ardhi za kijamii, kisheria na kitamaduni; uhakika na utekelezaji wa sheria kuhusu ardhi;

c. Kuelewa mfumo wa dhamana ya umiliki wa ardhi ikiwa mpango huo unawezesha kutoa nafasi ya kukabili matatizo yanayokabili mfumo uliopo wa umiliki wa ardhi;

d. Sababu zinazochangia ukosefu wa ulinzi katika mfumo wa umiliki wa ardhi katika baadhi ya makundi ni kuwa baadhi ya makundi hayawezi kuwa sawa kama kwa mfano kwa wanaume, wanawake, walemavu/makundi yalio na upungufu, watu wa kiasili, wanaoishi misituni, jamii za wafugaji, na jamii za uvuvi.

e. Usimamizi wa ardhi unajumuisha uhusiano wa kijamii na pia unaonyesha mfumo wa mamlaka, dhamana ya kiuchumi, kanuni za kijamii, maana hali ya kitamaduni na mara nyingi mpangilio unaonyesha mpangilio wa ukosefu wa usawa.

f. Ulinzi wa umiliki wa ardhi (kisheria na kitaasisi) na kuongozwa mara nyingi na wanaume katika familia wakichukuliwa kuwa wameaminiwa na haki zote nyumbani kwao. Huenda hali isiwe hivyo kulingana na maelezo ya sura inayofuata,

g. Kwa wnawake haswa mila zinaweza kuwazuia kwa misingi ya; **nini nani, vipi, lini, wapi** na **kwanini** wanastahili kuwa na haki ya kumiliki ardhi, na

h. Mfumo wa umiliki wa ardhi wenye dhamana unaoambatana na utata wa jinsia.

Kulainisha tofauti za kijinsia na uwezeshwaji wa wanawake ni suala ambalo linaendelea kuwa jumuishi katika ulimwengu wa maenedeleo. Kuendelea kuwepo kwa ubaguzi wa kijinsia kwa mjibu wa ardhi kunalemaza juhudi za kuhusisha kila mmoja kwa maendeleo na uongozi bora. Miingilio yote kwa haki kuhusu ardhi inatakiwa kushughulikia ubaguzi wa kijinsia katika sehemu hii.

**Sanduku 1:0 Haki za umiliki ni zipi?**

Tunaposikia haki kuhusu mali mara nyingi tunafikiria umiliki. Neno "mali" limetokana na jina la kilatina linalomanisha umiliki. Ufafanusi wa haki za umiliki wa ardhi uibua changamoto tofauti ndiposa nivigumu kueleza maana yake hasa kwa wanawake, vijana, makundi yaliyotengwa katika jamii na hata walemavu.

Wanotaka kumiliki ardhi huwa na hamu ya kupata hati miliki (inayojulikana kama "title deed") na pia mfumo wa ukodishaji, ruhusa ya kutumia ardhi, leseni, haki za kuchimba madini na matakwa mengineo. Wamiliki wa ardhi hutarajia kutumia kikamilifu ardhi yao na kujiendeleza bila muingilio kutoka kwa serikali au kwengineko. Wamiliki vilevile wanatarajia kuweza kumuondoa yoyote kutoka kwa ardhi yao na kuiuza kwa yeyote wanayetaka kumuuzia na katika masharti yao wenyewe.

Kumiliki kwa ardhi kunahusisha haki na majukumu. Haki hizi na majukumu zinatofautiana kulingana na nchi na hata kimkoa au kulingana na jinsi sheria imeelezea na kuzilinda haki hizo. Ukuaji wa wanawake katika maendeleo ya kiuchumi na haki zao katika kumiliki ardhi vinahusiana.

'Haki kuu za kumiliki mali na ardhi – ikiwa ni katika mazingira ya kitamaduni ama rasmi– inasimimia kama namna zote za kupata mwanya kiuchumi [2] kwenye masoko makuu na kupata mwanya kijamii hadi taasisi zisizokuwa na soko kama familia na jamii – mifumo ya usawa wa uongozi' (Giovarelli, 2007: 195). Katika hali hii hoja zinazotokana na umiliki wa ardhi ulikuwa na umuhimu mkubwa na kwa maisha ya wanawake na masuala yafuatayo ni muhimu.

Marekebisho ya kisheria katika sera za umiliki ya ardhi hivyo basi yanatakiwa kuondoa ubaguzi wa kijinsia wa haki za kumiliki mali. Hii inaweza kufanyika kwa namna zifuatazo:

(a) Kutambua sababu za kijamii na kitamaduni ambazo huwazuia wanawake kupata haki zao za kumiliki ardhi katika kaunti zote 47 kote nchini Kenya.

(b) Kuandaa sheria ambayo itashughulikia uhalisia wa desturi za kitamaduni na pia kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wana haki ya kumiliki mali,

(c) Kutengeneza na kutekeleza mipango ya kijamii na kitamaduni ambaye itawasaidia wanawake kuepuka vikwazo na kufahamu haki zao za kumiliki ardhi.



2 Kupata ardhi kunaathiri karibu sehemu zote za maendeleo ya sera. Kwa mfano ina uhusiano wa moja kwa moja mazao ya kilimo na kuhakikisha kuwa kuna



"*Dunia ambayo ni nzuri kwa wanawake ni nzuri kwa kila mtu*"
*(Wellesley Centers for Women)*

# Sehemu ya 2: Kwa nini wanawake wapate ardhi

## 2:0 WANAWAKE NA UMILIKI WA ARDHI

ULIMWENGUNI KOTE, kutokuwa na usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi na raslimali nyenginezo kunahusishwa na umasikini wa wanawake na kutengwa kwao katika jamii. Vikwazo vinavyowazuia wanawake kimiliki ardhi inavyofaa ni vikubwa na hujitokeza katika miktadha Fulani. Kwa mfano, Kenya ina jumla ya watu karibu milioni arobaini na tatu (43). Asilimia 51% yao wakiwa wanaume na asilimia 49 % ni wanawake . Kilimo na ufugaji ndio kitega uchumi kikuu katika sehemu za mashambani nchini Kenya ambako asilimia 85% ya wanaofanya kazi hizo ni wanawake. Isitoshe, sekta ya kilimo huchangia asilimia 30 % ya uchumi wa Kenya (Pato la kitaifa la uchumi). Kunazo sababu nne muhimu za kutetea haki za wanawake:

a. Haki za kibinadam za wanawake zimekiukwa
b. Wanawake hawatambuliwi katika jukumu lao kubwa la kuzalisha chakula na kuthibiti mali asili
c. Mabadiliko katika mazingira yanashinikiza kufikiriwa upya kwa ardhi kama raslimali ya kudumu na jinsi ardhi na mchanga unavyopoteza rotuba kama changamoto zinazokabili maendeleo ya kudumu.



Huku haki zikiwa zimepitishwa katika mifumo ya kisheria inayohusu makundi fulani kupata ardhi (kwa mfano wenyeji wa zamani kwa kiwango fulani ,wanawake )baadhi ya haki za umiliki zimeathiriwa na jambo la kupata ama kukosa ardhi (kwa mfano kupatikana makazi,chakula,maji, kazi)na sera katika sheria za kimataifa zinatoa ulinzi kuhusiana na kupatikana kwa ardhi (kwa mfano usawa na

kutokuwepo kwa ubaguzi katika umiliki na urithi ),basi kuzingatiwa kwa kina kwa athari za kisheria katika maswala ya ardhi kuhusu haki za kibinadam ni muhimu (Wickeri and Kalhan ,2010)

Uhusiano wa jinsia kulingana na tamaduni na vilevile jamii zinawapa wanawake uwezo mdogo wa umiliki wa ardhi kuliko wanaume. Uhusiano baina ya wanume na wanawake katika muktadha wa ardhi pia unategemea hadhi katika jamii katika uwezo wa kifedha ama umasikini, jinsi mtu anavyojuana na wengine katika jamii, umri na hata kabila. Mbinu za kupata ardhi na umiliki wa ardhi pia zinatofautiana kulingana na kabila, eneo na aina ya ardhi hiyo (mashambani au mijini).
Tamaduni ndizo huamua ugavi wa majukumu ya kikazi katika maeneo ya mshambani kando na kuamua jinsi ya kuendesha shughuli za kilimo na maamuzi ya kifamilia vilevile urithi wa mali. Kupigania haki za kijinsia kunahitaji kuelezwa kwa nini kazi zinazofanywa na wanaume na wavulana zinafa kuwiana wala sio kwenda kinyume cha mapambano ya wanawake kote duniani kujikomboa, barani Afrika na katika maeneo wanakotoka (Ratele, 2008)



Kwa kawaida wanawake wamekuwa tu na haki isiyokuwa halisi ama 'inayotegemea kitu fulani' kumaanisha kuwa wanastahili haki zao kwa niaba ya watu wa kiume katika familia. Hivyo basi wanawake hupoteza haki zao kutokana na talaka, ujane ama wanaume wao kuhama. Ushahidi wa utafiti unaonyesha kuwa vipande vya ardhi wanavyomiliki na kina wanawake huwa na thamana ndogo.


Wanawake katika jamii za wafugaji hawana haki za kumiliki ardhi na hawana uhuru wa kujistawisha kiuchumi kama wanaume. Katika jamii hizi wanawake wametengewa aina Fulani tu ya mali ambayo wanweza kutumia. Hata hivyo mahitaji ya kimsingi ya wanawake yanaonekana kupuuzwa katika utamaduni wao unaopendelea wanaume. Haki za wanawake kuhusu rasilimali zinapitia kwa wakoo wao wa kiume (mume,baba, kaka, mjomba, binamu na kadhalika.) Hizi nguvu za ziada anazopata mwanaume huwafanya wanawake kutokuwa na uwezo wa kutoa maamuzi kuhusu kupata na/ kuthibiti mali. Hii imedhaifisha nafasi ya wanawake na kuathiri uwezo wao wa kuendelea kusimamia rasilimali ambazo ziko mikononi mwao kwa jina tu. Kutokana

na mabadiliko mengi kufanyika nafasi ya wanawake katika kusimamia rasilmali inazidi kuwa hatarini. Manufaa ya kiuchumi yanatokana na mapato kutoka kwa ardhi na jukumu la ardhi kama dhamana. Manufaa ya kijamii yanapatikana katika viwango vya familia na jamii na kuboresha uwezo wa kujipigania katika kila familia huongeza dhamana wakati mtu anazeeka mbali na kuongeza uwezekano wa kushiriki katika makundi ya kijamii

**Namna wanawake walivyohusishwa Kenya**


1. Ni 5% pekee ya ardhi yenye hati miliki ambayo inamilikiwa kwa pamoja na wanaume na wanawake;
2. Ni 1% pekee ya hati miliki za ardhi ambayo inamilikiwa na wanawake pekee;
3. 89% ya kazi zinazofanywa ili kukidhi mahitaji inatolewa na wanawake;
4. 70% ya kazi inayotumika kuzalisha mimea inayouzwa inatolewa na wanawake;
5. Karibu 32% ya familia zinaongozwa na wanawake;
6. Wanawake wanapotumia ardhi huwa kuna chakula cha kutosha;
7. Ukosefu wa haki za kumiliki mali kama vile ardhi miongoni mwa wanawake huchangia kupunguza mazao yanayotokana na kilimo, kukosa ajira na kuwepo kwa umasikini vijijini katika kaunti mbalimbali. Katika matukio mengine, wanawake wamekuwa wakipoteza ardhi ardhi zao ikiwa maamuzi yote kuhusu matumizi na umiliki wa ardhi yanafanywa na wanaume.

**Mchoro: 2:0 Vikwazo katika umiliki wa mali**



Japokuwa mifumo ya kitamaduni inazidi kubadilika, hiyo haiashirii habari njema kwa wanawake. Uwajibikaji wa machifu na wazee wa kitamaduni wa wa jamii hizo wanazidi kugawanyika; mifumo ya ukoo inazidi kufifia na kuacha ardhi kusimamiwa na wanaume wachache ama na familia. Hii inamaanisha mamlaka, usimamizi na maamuzi yanaongozwa na wanaume. Athari ya moja kwa moja ya mpango huo ni kuwa wanawake wanakosa uwezo wa kutoa maamuzi kuhusu ardhi

**Mchoro 2.1: Haki za wanawake za kumiliki ardhi zilizozilindwa**




Chanzo: Giovarelli & Scalise (2015) 3

**Masuala ibuka Kwa wanawake**

a. Utandawazi wa kilimo cha biashara;
b. Teknolojia mpya; kukuza mimea kisayansi na athari zake kwa wanawake;
c. Kubinafsisha raslimali hali na kuthibiti bidhaa za umma kutoka kwa serikali hadi kwa mikono ya watu binafsi, kwa kuwatenga wanawake kwa kiasi kikubwa;
d. Unyakuzi wa ardhi ambapo serikali za kitaifa na kigeni; kampuni za kimataifa hupata ardhi na kuikuza kwa watu wake ama kwa soko la nje;
e. Ubaguzi katika kupata habari,na kupata mafunzo kuhusu mifumo ya teknolojia;
f. Mizozo na athari zake katika haki za kumiliki ardhi katika maisha ya wanawake



3 Utaratibu wa mfumo wa umiliki wa ardhi kwa wnawake kwa Uchambuzi : LanHaki za wanawake

Kupata nafasi sawa katika ardhi, kusimamia Na kumiliki ni viungo muhimu kwa kunaleta athari kubwa muhimu ya matumizi (kuongeza gharama ya chakula, maslahi ya watoto na elimu) na uzalishaji haswa kwa nchi ambazo wanawake wanahusika katika maswala ya ardhi kwa wingi.Juhudi zote za wanawake kupata ardhi, kwa misingi ya kanuni na taratibu kuzingatia jinsia ambazo zinatakiwa kujumuisha wanawake kuwa na haki sawa za kumiliki ardhi. Hata hivyo kuna desturi inayoendelea ya kuwa na pengo kubwa kati ya haki za kurithi zilizowekwa kwenye Katiba, sheria za ardhi, sheria za familia na kufahamu ukweli kuhusu wanayopitia wanawake .[4]

## 2:1 WANAWAKE KURITHI ARDHI

KUHAMISHA MALI kama vile ardhi ndani ya familia kunatakiwa kuonekana na kupimwa kwa muktadha wa kitamaduni na kuhusisha taasisi za kijamii kama 'masoko ya ndoa'. Maana iliyowekwa katika umiliki, kutumia na kupata ardhi inaonekana kuwa na utata huku tofauti za kijinsia zikionekana kuhusu jinsi watu binafsi wanavyochukulia haki za kumiliki ardhi wanazopata.

Katika kufahamu uhusiano, Quisumbing (2007) anathmini jinsi ya kuhamisha mali (inayojumuisha ardhi) kwa watoto wao na vizuizi wanavyopitia watu wasiojiweza wakati wa uhamisho huo.

**Jedwali 2:0 Sababu zinazokubali ama kuzuia kuhamisha mali katika vizazi mbalimbali vya familia.**

| | KUJENGA UHUSIANO | VIKWAZO |
|---|---|---|
| **Mapenzi** | Wazazi hujali maslahi ya watoto wao wanakua. | Mzazi anaweza kupendelea namna tofauti ya vile mtoto anaweza kuwekeza. Uhaba wa rasilimali hufanya hali ya kubadilisha kuwa rahisi. |
| **Faida** | Wazazi hutathmini kiwango ambacho uwekezaji utawafanya watoto wao (ama wenyewe) kuwa bora kwa siku zijazo katika kufanya maamuzi ya kuwekeza. | Manufaa ya kupata wafanyikazi katika taasisi ya ndoa hali kadhalika kuwasaidia wazee yanaweza kutofautishwa baina ya watoto na inaweza kuathiri namna tofauti ya wazazi kuwekeza kwa watoto wao. |



4 Mada ya haki za wanawake kuliki ardhi na sheria inapatikana katika chapisho la pili ambalo bado linaandaliwa na kurugenzi ya Utafiti– NLC.

| | KUJENGA UHUSIANO | VIKWAZO |
|---|---|---|
| **Masharti** | Uwekezaji wa wazazi kwa watoto wao huwa na masharti ya wao kutumia rasilimali (pesa, wakati) na gharama pia uwezo wao wa kubadilishana kwa kuzingatia uwekezaji wa baadaye. | Watu wasikokuwa na rasilimali za familia huwa na upungufu (kwa mfano familia inayoongozwa na mwanamke). Kuwepo na masharti mengi kunamaanisha kuwa makubaliano yanatakiwa kuzingatiwa wakati matokeo yanapokuwa mabaya. |
| **Ushawishi** | Tofauti zilizopo za ushawishi kati ya wazazi na jamaa huathiri uwekezaji huu. | Wakati wa kutekeleza nguvu za ushawishi mzazi anaweza kutoa uamuzi wa nyumbani[5] kwa njia isiyoridhisha kuhamisha mali hadi kwa watoto (haswa wasichana na wale wanaoishi na ulemavu), ama kwa baadhi ya watoto kuzidi wengine. Hii inaweza kuleta ubaguzi wa wazazi kupendelea wengine |

Hivyo basi baadhi ya maswali yataulizwa jinsi ifuatavyo:

**Je imekuwa vigumu kwa wanawake kuungana na kutetea haki zao kibinafsi kuhusu ardhi?**

a. Kiini cha kuelewa ndoa na urithi katika jamii tofauti kwa muda ni kutambua (endapo jamii hiyo inapendelea wanaume ama wanawake).

b. Wanawake mara nyingi hawaruhusiwi kurithi ardhi ikidhaniwa kuwa wana mikosi. Wale ambao ni wajane, mayatima, ambao hawajaolewa, waliopata talaka ama ni tasa wana shida kubwa sana. Wale walio katika ndoa za zaidi ya mwanamke mmoja pia wanaweza kuathirika vibaya.

c. Katika miktadha mingi ya kitamaduni umiliki ama utumiaji wa ardhi unatambulishwa moja kwa moja na jinsia ya kiume. Ili kupata ardhi wanawake wanahitaji msaada mkubwa kutoka kwa serikali pamoja na hatua ya kuhalalisha kudai kwao kwa ardhi.



5 Suala la familia ni kati ya masuala magumu mno kutafiti. Hata hivyo kutoa uamuzi ndani ya familia ni moja ya sehemu ambazo sauti ya wanawake haisikiki.

d. Kurasmisha mipango kati ya wanandoa huwa muhimu kukabili matatizo yanayosababishwa na mashemeji wakati mume anapofariki (Tazama kisanduku 2:0 chini).
e. Wanawake wanaweza kuwa na wasiwasi kushirikiana ama kupigania haki zao kibinafsi za kumiliki ardhi kwa sababu ya kuwepo katika jamii ya wanaume ambao ndio huamua kutoa baadhi ya manufaa ya bidhaa ama yasikuwa ya bidhaa.
f. Japokuwa kuna tofauti baina ya nyumba mbalimbali kuhusu upatikanaji wa rasilimali ambazo zimeorodheshwa haimanishi kuwa hadhi ya mwanamke ya kuwa mtu mzuri haiwezi kuhusishwa na ya mumewe ama baba.
g. Maslahi ya wanawake na wanaume katika ndoa ndani ya ndoa ni jambo la pamoja na vile vile la kutenganishwa hivyo basi kufanya suala la mapambano ya kijinsia kuwa nyeti mno. Hii ndiyo moja ya sababu ambazo kuwa na hati ya pamoja imekuwa njia bora ya kuziba pengo kuhusu umiliki wa mali kwa kuzingatia jinsia (Kwa mfano katika mataifa mengi kilatini).

**Kisanduku 2:0 Fahamu haki kuhusu ardhi**

Mzee Zakayo alinunua ekari (20) za ardhi ambapo aliishi na mkewe Tina na watoto wao wanane (wavulana 4 na wasichana 4 ) na wakaimarisha ardhi hiyo kwa miaka 35. Kabla afe Zakayo aliwaambia wazee wa ukoo wake kuhusu uamuzi wa mkewe na watoto wake wanane kurithi ardhi yake ya ekari 20 ambayo ilikuwa imefanyiwa kazi nyingi. Miongoni mwa wavulana wake, wawili walikuwa walemavu na alitaka walindwe kutokana na mapato yaliyokuwa yakizalishwa katika ardhi hiyo. Baadaye aliandika wosia kuunga mkono kauli yake. Hata hivyo akiwa bado hajaoa Tina, alipata watoto wawili wa kiume ambao ndio waliokuwa wa kwanza. Miaka kumi na mitano kabla ya yeye kufariki alikuwa amegawanya ekari tano kwa wavulana hao ambao waliweka makazi yao hapo. Pindi tu baada kifo cha Zakayo, hao wavulana wake wawili wakubwa walienda mahakamani kupinga kiwango cha ardhi walichopewa na wakamshtaki mama yao wa kambo Tina kwa kuathiria uamuzi wa baba yao marehemu. Kufikia 2014, kesi ilikuwa ndani na nje ya mahakama kwa miaka 14 na bado haikuwa imetatuliwa **( Chanzo: Kazi ya nyanjani kaunti ya Trans-Nzoia 2015)**

Masuala yaliyoangaziwa katika kisanduku 2:0 hapo juu zinaonyesha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kukabili miktadha ya kurithi ardhi kitamaduni na kisheria. Kwa mujibu wa Giovarelli na Scalise (2015) masuala muhimu ya kuzingatia ni:

a. Kuelewa kuwa haki za kumiliki ardhi katika sheria za kitamaduni zinaweza kubadilishwa ikiwa hali ya mwanamke imebadilika kulingana na umri, hadhi yake ya kiuchumi na kijamii, nafsi katika familia na/ ama jamii, ndoa ya mke na mume mmoja ama ndoa ya wake wengi ama ndoa ya Kiislamu;
b. Kuelewa kuwa kanuni nyingine za kando zinaweza kuathiri haki za wanawake kumiliki ardhi. Zinajumuisha umiliki wa pamoja wa mali, dhana ya kitamaduni kuhusu wanawake na umri wa kisheria wa ndoa;
c. Kuelewa vizuizi vilivyopo katika kutekeleza haki zilizopo katika sheria, kama vile kutokuwepo kwa majina ya wanawake katika hati miliki, muda na mwendo hadi katika mahakama rasmi;
d. Kuelewa kuwa haki katika sheria ya kitamaduni inaweza kubadilika ikiwa nafasi ya mwanamke itabadilika; na
e. Kutambua jinsi majukumu ya kijamii ya jinsia yanaweza kuathiri namna wanawake wanavyoweza kutekeleza haki zao.

### 2:2 Na je sauti za wanawake zasemaje?

Yafuatayo ni matukio mawili ambapo haki za wanawake kumiliki ardhi zimekiukwa:

**SANDUKU 1**

**A Sian Mkulima (mjane – Kaunti ya Narok)**

**Sian:** Nimepelekwa mahakamani na watu fulani wnaosema ninaishi katika ardhi yao.

**Mtafiti:** Hii ilitokea vipi?

**Sian:** baada ya mume wangu kufariki, nimekuwa katika ardhi yangu kwa miaka 28 na kuifanyia ukulima. Kisha barabara ya zamani iliyokuwa ikipitia karibu na nyumba yangu, lami ikabambuka kabisa na watu wakaanza kutumia ardhi yangu, wanapitia ndani ya ardhi yangu. Na huyo Chifu! Huyo mwanamume! Aliniambia nimechukiua shamba la mtu na wanataka niondoke, vipi tena? Kile nilichosalia nacho ni kidogo kuliko alichoniachia na watoto wangu mume wangu.

**Mtafiti:** Na je umejaribu kutatua suala hilo?

**Sian:** Kujaribu? Kwani husikii nimeenda kortini kwa hili suala la kuingia kwa ardhi yangu kinyume cha sheria? Nilijaribu wazee wakaniambi 'mwanmke wewe fuata maagizo wewe ni mgumu sana'

**Mtafiti:** Kwa hivyo utachukua hatua gani nyengine?

**Sian:** Nataka usaidizi. Nitatafuta msoroveya na wakili wangu mwenyewe, na tuone nitakapofika kwa sababu wazee hawawezi kusaidia.

**Mtafiti:** Taratibu za mahakama zinaweza kuchukua muda, je nini kitafanyika katika ardhi yako?

**Sian:** Nimefadhaishwa sana, hawa watu wanataka kunipokonywa shamba langu mchana tu

**SANDUKU 2**

**Nanjala Mwalimu (Mwanamke aliolewa) – Kaunti ya Bungoma**

**Nanjala:** Wanaume wengi katika sehemu hii wamerithi ardhi kutoka kwa kina baba wao ikilinganishwa na wachache waliojinunulia

**Mtafiti:** Suala la kurithi katika Kaunti hii dhahiri kuwa hati miliki nyingi ziko katika majina ya kina baba; sababu ni kwamba wengi wao hufikiria kuwa utaratibu huo ni ghali mno na kuna mpangilio mrefu na kizazi cha zamani husali na hati miliki kwa sababu wanadhania kizazi cha sasa kitauza ardhi

**Nanjala:** Makundi mbalimbali ya wanawake(walioolewa, waliopata talaka, wajane na walemavu) huku watoto wakiwa na haki ya kurithi ardhi kupitia kwa watoto hasa wavulana huku wale ambao hawakuwa na watoto wakiwa na haki za kuzika pekee pembeni mwa ua. Asili mia kubwa ya wanawake hawafahamu haki zao za kikatiba lakini walio na ufahamu husema kuwa hawawezi kupigania haki zao kwasababu hawana uwezo wa kiuchumi kupeleka kesi mahakamani

**Mtafiti:** Je una mifano ambayo unayoweza kutoa?

**Nanjala:** Nitakupa mfano ambapo mwanaume aliwapa wasichana wake urithi lakini watoto wake wa kiume ambao walikuwa wamemakinika walipigania haki yao na wasichana hao wakabadilisha nia yao na kutulia kuzuia mgongano baina ya watu familia hiyo. Mwanaume huyo alisema ... 'je mjane anawezaje kupewa ardhi wakati ana nafasi ya kuolewa kwengineko? Kakake marehemu anatakiwa kuweka hati miliki hiyo watoto wakiwa bado wachanga kwa sababu mjane anaweza kuuza



*“Mtu anayeomba nguo haoni fahari kucheza” (Methali ya Igbo)*

# Sehemu ya tatu: Mafunzo kuhusu Sera na desturi

## 3:0 MUHTASARI

DHAMIRA YA uchapishaji huu si kufifisha miradi na mipango inayoambatana uhusiano wa kijinsia. Badala yake inaonyesha mabadiliko yaliyotengenezwa na manufaa ya malengo asili. Hali ya ardhi ni tata sana nchini Kenya na inahitaji kuangalia vikwazo vilivyopo katika kiwango cha chini(sheria na sera), mipangilio ya kitaasisi (mbinu na taratibu za usimamizi wa ardhi), na mabadiliko katika mazingira ya kawaida (makundi ya kijamii ambayo ni maarufu na sababu zinazoambatana na imani za kijamii, kanuni na desturi za kitamadani). Hivyo basi kiwango cha jamii kinatakiwa

## 3:1 MIKAKATI BORA YA MABADILIKO

ILI KUFIKIA haki za wanawake kuhusu ardhi wanatakiwa kulindwa na sheria na desturi na zifuatazo ni hataua nne zinazostahili kufuatwa.

### A. Mapendekezo ya Sera

- Marekebisho ya kisheria yanatakiwa kufanywa kuhakikisha kuwa haki za urithi wa mali zinatekelezwa bila kupendelea jinsia yoyote;
- Ongeza masharti ya ulinzi kuhakikisha kuwa wanawake wanaelewa haki zao kama wamiliki;
- Boresha mfumo wa usaidizi wa kisheria na mbinu bora za kusambaza maelezo

kuhusu haki za kisheria;
   - Serikali kutoa msaada mkubwa kwa wajane ambao hawana namna ya kujisaidia;
- Kuweka mikakati ya kuwalinda wanawake kuhakikisha kuwa wanajishughulisha;
- Utafiti na tathmini ya jinsia – katika hatua ya kukabili tatizo la ukosefu wa taarifa muhimu kutekeleza marekebisho na dhana za mabadiliko;
- Haki za wanawake kuhusu ardhi zinatakiwa kuchukuliwa kama haki za kimsingi za binadamu; na
- Haki za makundi yaliyotengwa kijamii zinatakiwa kuwa sehemu ya kusuluhisha matatizo ya kulinda haki za kijinsia – na kung'oa mizizi iliyokita ya taasisi zinazowapendelea wanaume katika mielekeo, desturi na sera.

**B. Kuwezesha sheria kuwafaa wanawake**

- Kuwatambua wanawake kama wafaidi wa moja kwa moja wa ardhi na mifumo iliyorekebishwa ya ardhi bila kujali ikiwa wameolewa au la;
- Kuzuia desturi za kitamaduni ambazo zinabagua;
- Kuharamisha wajane kukosa urithi na watoto walioachwa;
- Kutoa nafasi sawa ya urithi kati ya wavulana na wasichana;
- Kutambua ndoa za kitamaduni ambazo zinakubali usawa wa haki kati ya mume na mke walioona;
- Kutambua haki za wanawake kumiliki na kuthibiti mali yao wenyewe;
- Kutambua kazi ya wanawake na michango yao katika kupata mali hata kama si kwa kutoa pesa;
- Kuwe na usawa katika kugawanya mali iliyopatikana wakati wa ndoa baina ya wahusika kukitokea talaka, utengano ama kifo (wajane na mayatima);
- Kutambua umiliki wa pamoja na usimamizi wa mali iliyopatikana wakati wa ndoa na kumiliki boma bila kupingwa mwanandoa moja anapofariki.

**C. Kuwekeza katika utekelezaji**

- Kutafiti na kukusanya ushahidi kuhusu mipango itakayofanya kazi; utafiti unatakiwa kulenga mapengo kama vile uhusiano uliopo kati ya ardhi, kuhama na jinsia; UKIMWI na haki kuhusu; maskwota na haki zao za ardhi; ukiukaji wa haki za kumiliki mali;

- Kukusanya data na ushahidi ulioratibiwa kuhusu mbinu bora za kuingilia kati kwa matokeo na kuhakikisha kuna haki za kumiliki mali;
- Toa uhamasisho zaidi na mfunzo ili kutoa msingi wa kutekeleza mkakati wa sheria ama marekebisho yoyote ya sera;
- Ensure rights holders know about and are able to claim their rights;
- Kuhamasisha na kuwawajibisha maafisa wa serikali na wakuu wengine kama vile majaji, majaji, maafisa wa utawala, polisi, viongozi wa jamii, na mawakili;
- Kushirikisha vyombo vya habari ni muhimu haswa na taasisi zinazotoa mafunzo
- Kutafuta ufumbuzi kwa ukiukaji wa haki;
- Kutoa nafasi kwa upatikanaji wa haki kwa kuunganisha huduma kama vile utunzaji wa afya na huduma za kisheria.
- Kuimarisha uwezeshwaji wa wanawake, kwa kuwaunga mkono kupinga uhusiano wa mamalaka yasiyokuwa na usawa na kuwahimiza kujiona kama walio na haki sawa na wanaume.
- Kupinga desturi kandamizi mahakamani.

**D. Kufanya mabadiliko katika kiwango cha chini**

- Kujihusisha na mifumo ya haki za kitamaduni na kuhusisha jamii katika kuratibu ramani na stakabadhi ambayo huyawezesha makundi ya wanawake wa mashinani kuandika kuhusu ufahamu wa jamii katika masuala ya ardhi;
- Kubuni miradi ambayo itachochea utetezi na mipangilio ya kuchukua hatua;
- kutoa mafunzo kwa makundi yanayotekeleza ufuatiliaji katika jamii na wanasheria kulinda haki za wanawake katika kiwango hicho;

# Marejeleo

Aliber, M., Walker, C., Machera, M., Kamau, P., Omondi, C. and Kanyinga, K., 2004, The Impacts of HIV/AIDS on Land Rights – Case studies from Kenya, Rome FAO, available online at http://www.fao.org/sd/dim_pe3/docs/pe3_040902d1_en.pdf

Benjaminsen, T.A., and Lund, C., (eds), 2002, Securing Land Rights in Africa, London, Frank Cass.

Birgegard, L.E, 1993, Natural Resource Tenure: A Review of Issues and Experiences with Emphasis on Sub-Saharan Africa, Swedish University of Agricultural Sciences, Uppsala.

Cabral, A., 1969, 'Brief Analysis of the Social Structure in Guinea,' in Cabral, Revolution in Guinea: An African People's Struggle, Stage 1. London, pp. 46-61.

Carney, D., 1998, Sustainable rural livelihoods: What contribution can we make? London: Department for International Development.

Cotula, L., 2002, Gender and Law: Women's Rights in Agriculture, Rome, FAO, Legislative Study 76.

Cotula, L., Toulmin, C., and Hesse, C., 2004, Land Tenure and Administration in Africa: Lessons of Experience and Emerging Issues, London, IIED.

Cousins, B., 1997, 'How Do Rights Become Real? Formal and Informal Institutions in South Africa's Land Reform', IDS Bulletin, Vol. 28, No. 4, pp. 59-68.

Fafchamps, M., and Quisumbing, A.R., 2002. 'Control and Ownership of Assets Within Rural Ethiopian Households', Journal of Development Studies 38(6): 47–82.

Giovarelli, R., 2007, 'Gender and land tenure', in Posterman, R.L., Mitchell, R., and Hanstad, T. (eds) One Billion Rising, Leiden university Press, Leiden.

Gluckmann, M., 1969, 'Property Rights and Status in African Traditional Law,' in Gluckman, M. (ed), Ideas and Procedures in African Customary Law, Oxford

University Press.

Ikdahl, I., Hellum, A., Kaarhus, R., Benjaminsen, T., and Kameri-Mbote, P., 2005, Human Rights, Formalisation and Women's Land Rights in Southern and Eastern Africa, Oslo, available online at http://www.jus.uio.no/ior/kvretten/kvrett_skriftserien/dokumenter/ noradrapport.pdf.

Katz, E., 1997, The Intra-household economics of voice and exit, 3(3) Feminist economics 25-46.

Lu, T., Zwicker, L., Kwena, Z., Bukusi, E., Mwaura-Muiru, E., and Dworkin, S,L., 'Assessing barriers and facilitators of implementing an integrated HIV prevention and property rights program in Western Kenya,' AIDS Education and Prevention, Volume 25, Issue 2, April 2013, pp. 151–163.

Migot-Adholla, S.E.,Place, F., and Olusch-Kosura, W., 1994, 'Security of tenure and land productivity in Kenya'. In J. Bruce and S. E. Migot-Adholla (eds). (1994) Searching for land tenure security in Africa. Iowa: Kendall/Hunt.

Mitchell, R., 2007, 'formalization of rights to land', in Posterman, R.L., Mitchell, R., and Hanstad, T. (eds) One Billion Rising, Leiden university Press, Leiden.

Posterman, R.L., Mitchell, R., and Hanstad, T. (eds) 2007, One Billion Rising, Leiden University Press, Leiden.

Quisumbing, A. R., and McClafferty, B., 2003, Using gender in research development, International Food and Policy Research Institute.

Tsikata, D., 2003, 'Securing Women's Interests within Land Tenure Reforms: Recent Debates in Tanzania', Journal of Agrarian change, Vol.3, Nos.1 & 2.

## NOTES

design layout: frankosango@gmail.com

## CONTACT US

NATIONAL LAND COMMISSION

Ardhi House, 12th Floor, 1st Ngong Avenue, - Off Ngong Road,

P.O. Box 44417 – 00100, - Tel: +254-2-2718050, Nairobi, Kenya

-Email: info@landcommission.go.ke, Website: www.landcommission.go.ke

ISBN 978-92-5-009527-1

9 789250 095271

I6501SW/1/05.17

This publication has been produced with the assistance of the European Union. The contents of this publication are the sole responsibility of FAO and can in no way be taken to reflect the views of the European Union.